**Daraja la Magufuli**
**Alama ya Uhandisi na Hatua Mpya katika sekta ya Miundombinu Tanzania**

Tanzania imeshuhudia uzinduzi wa Daraja la John Pombe Magufuli mnamo tarehe 19 Juni 2025. Hii hatua kubwa katika historia ya maendeleo ya miundombinu nchini mwetu. Kwa mtaalamu wa ujenzi, mafanikio haya si tu fahari ya kitaifa bali pia somo kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## Ubora wa Kiufundi na Utekelezaji

Tangu kuanza kwale mradi wa Daraja la Kigongo Busisi na atika kila hatua, kuanzia upimaji wa awali, usanifu, hadi ujenzi mradi huu umeonyesha weledi mkubwa katika maeneo yafutayo, kwa uchache:

- Uhandisi wa daraja refu (3.2 km) juu ya maji na kulifanya liwe daraja refu Afrika Mashariki na Kati.
- Ujenzi wa barabara ya mifereji minne na njia yenye kubeba vyombo vya moto 1600 kwa mara moja na 12000 kwa siku, pamoja na njia za waenda kwa miguu.
- Miundombinu inayohimili uzito wa hadi tani 180, kwa ajili ya mizigo mikubwa ya kanda ya ziwa.

Mradi umefadhiliwa kikamilifu na Serikali ya Tanzania kwa zaidi ya shilingi bilioni 716, bila mkopo wa nje. Hii ni ishara ya uwezo wa ndani wa kitaifa kusimamia na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo.

## Ajira, Ujuzi na Ushirikishwaji wa Wazawa

Zaidi ya **Watanzania 34,000** walishiriki moja kwa moja katika mradi huu. Tumejifunza:

- Ujenzi wa madaraja kwa kutumia teknolojia.
- Mbinu za usafirishaji salama wa vifaa kwenye mazingira ya ziwa.
- Usimamizi wa mazingira na ikolojia ya majini.

Mradi huu umeacha urithi wa kiufundi na maarifa ambayo yatafaidi sekta ya ujenzi kwa muda mrefu.

## Kichocheo cha Maendeleo

Kupitia daraja hili:

- **Biashara zitakua**, gharama za usafirishaji zitapungua kwa sekta za kilimo, uvuvi na madini nk.
- **Utalii na uwekezaji** vitaimarika katika Kanda ya Ziwa.
- **Huduma za kijamii** kama afya na elimu zitapatikana kwa urahisi zaidi.
- **Usalama barabarani** na ufanisi wa usafirishaji utaongezeka.

Huduma za kivuko sasa zitapelekwa kwenye visiwa vya pembezoni, na hivyo kuongeza uwiano wa maendeleo kwa jamii zilizokuwa zimejitenga.

*Nikimnukuu Rais Samia Suluhu Hassan aliitaja daraja hili kuwa ni "Daraja la Fursa."*

**Zaidi ya Daraja: Ni 'Ono' la kimkakati na urithi usioisha**
Mbali na kurahisisha usafiri kati ya Kigongo na Busisi, daraja hili limeondoa utegemezi wa kivuko, na limepunguza muda wa safari kutoka zaidi ya dakika 30 hadi chini ya dakika 5. Linaiunganisha Tanzania na majirani kupitia barabara kuu ya kimataifa.

Zaidi ya hayo, **Daraja la Magufuli ni ishara njema ya uwezo wa kitaifa wa kihandisi**. Linathibitisha kuwa hakuna kinachoshindikana pale ambapo maono ya utashi wa uwekezaji vinakutana pamoja,tena kwa weledi na utaalamu '*Heko Tanzania*'

*Imeandikwa na Suma Mwaitenda: Mtalaam wa Mkadiriaje Majenzi na Mtatuzi wa Migogoro katika Ujenzi.*
*Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu Ardhi*
*Raisi: Jukwaa la Wanawake katika Miundo Mbinu Afrika*
*Makamu wa Raisi: Chama cha Wakadiraji Majenzi, Tanzania*
*Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Usimamizi Ujenzi ~ Chuo Kuu cha Johannesburg*